

# MTIHANI WA NYAHOKAKIRA AWAMU YA PILI

# KISWAHILI FASIHI

102 / 3 - Karatası ya 3

Julai 2024 – Muda: Saa 2 Dakika 30

Jina: ..... Namba ya usajili .....

Shule: ..... Mkondo: .....

Maagizo

- (a) Jibu maswali **manne** pekee.
  - (b) Swali la kwanza ni la **LAZIMA**.
  - (c) Maswali hayo mengine matatu yachaguliwe kutoka sehemu nne zilizobaki yaani Tamthilia, Ushairi, Fasihi Simulizi na hadithi Fupi.
  - (d) **Usijibu maswali mawili** kutoka sehemu moja.
  - (e) Majibu yote **lazima** yaandikwe kwa lugha ya Kiswahili.

## Kwa matumizi ya mtahini pekee

**A. RIWAYA YA NGUU ZA JADI – Clara M.**

**LAZIMA**

1. **Mimi ni mwanaume. Naweza kuoa wakati wowote na idadi yoyote ya wanawake. Shida iko wapi? Mwanamke akishaolewa basi! Yake yamekwisha hapo. Akae na kuitumikia jamaa yake bila kuulizaauliza.**
  - (a) (i) Eleza muktadha wa dondoo hili (alama 4)
  - (ii) Bainisha toni mbili zinazojitokeza katika dondoo hili (alama 2)
  - (iii) Dondoo hili linadhihirisha nafasi ya mwanamke katika jamii. Thibitisha kwa kurejelea riwaya ya Nguu za Jadi (alama 8)
- (b) Onyesha uozo unaoendelezwa katika asasi ya uongozi katika riwaya hii. (alama 6)

**B. TAMTHILIA YA BEMBEA YA MAISHA – Timothy A.**

2. “ Afadhali hao. Mjukuu wangu hatofautishi kondoo, mbuzi na mbwa. Wote hao kwake yeye ni mbwa! ( wanacheka)”  
“Inachekesha”
  - (a) Eleza muktadha wa dondoo hili. (alama 4)
  - (b) Eleza sababu zinazowafanya wajukuu wanaorejelewa kutoweza kutofautisha kondoo, mbuzi na mbwa. (alama 8)
  - (c) Jadili namna elimu katika Bembea ya Maisha imekumbwa na changamoto nyingi (alama 8)
3. Gongo liliyamega maadili yake kimyakimya na taratibu uwajibikaji ukawa umemponyoka na kuteleza kama sabuni ya pofu jingi na kumwacha na kisomo chake tu.
  - (a) Eleza muktadha wa dondoo hili. (alama 4)
  - (b) Changanua vipengele vya kimtindo katika dondoo hili. (alama 4)
  - (c) Tambua toni inayodhihirika kwenye dondoo hili. (alama 2)
  - (d) Jadili athari ya mabadiliko katika jamii ya Bembea ya Maisha. (alama 10)

**C. HADITHI FUPI – Lutomia na Wengine .**

4.
  - (a) “Naam, wakati umewadia sasa wa kupata historia ya mgeni wetu”
    - i. Fafanua maudhui matatu ambayo yaekuzwa kutokana na historia ya ‘mgeni’ (alama 6)
    - ii. Fafanua dhamira ya mwandishi wa hadithi hii. (alama 4)
  - (b) Matatizo yanayowakumba waja ni msiba wa kujitakia. Eleza ukweli wa kauli hii ukirejelea hadithi ya **Fadhila za Punda**. (alama 10)
5. Kabla mwanamke yule hajakiwasha kile kibatari, nilijitokeza mle mvunguni na maguo yangu meupe kama ya maiti nikaagua mwangwi mkali mfano wa parapanda ya siku ya kiama.
  - (a) Yaweke maneno haya katika muktadha wake. (alama 4)
  - (b) Bainisha mbinu mbili za kimtindo katika dondoo hili (alama 2)
  - (c) Onyesha jinsi itikadi ilivyomwezesha mlinda mzimu na wahenga waliotukuka kuwafanya wanakijiji kuogopa na kuamini mzimu wa kipwerere kiasi cha kutofanya mzaha na maeneo yale ambayo mzimu uliotea. (alama 10)

**D. USHAIRI**

**6. Soma mashairi yafuatayo kisha ujibu maswali (alama 20)**

**SHAIRI A**

1. Mbiu naipulizia, kwa wa hapa na wa ng'ambo,  
Kwani ngoja 'mesikia, inaumiza matumbo,  
Kwa upole sitafyoa, hata kama kwa kimombo,  
Yafaa jihadharia, maisha yasende kombo,
2. Maisha yas'ende kombo, kututoa yetu ari,  
Zingatia haya mambo, wetu walezi mukiri,  
Kuwa wana kwa viambo, huwa Baraka na kheri,  
Watunzeni na maumbo, msijezusha hatari
3. Msijezusha hatari, na nyingi hizi zahana,  
Wazazi haya si siri, mawi mnayoandama  
Twaeleza kwa uzuri, matendoyo yatumma,  
Watoto tunayo mlori, ni lini mtajakoma?
4. Ni lini mtajakoma, na pombe ziso halali?  
Sio baba sio mama, mbona ny'hamtujali  
Mwafa ja nzi twasema, mwatuacha bila hali  
Hangaiko acha nyuma, kwani hamuoni hili?
5. Kwani hamuoni hili, kila mwapigana  
Nyumbanizo hatulali, jehanamu tumeona,  
Mwatusumbua akili, twaumia tena sana  
Achene na ukatili, kwani upendo hamna
6. Kwani upendo hamna, kama mbwa mwatuchapa  
Mwatuchoma sisi wana, mioyetu yatupapa  
Pa kujificha hatuna, tumbaki tukitapa  
Maisha hamu hayana, tumevunjwa na mkifupa.
7. Tumevunjwa na mifupa, hata leo uke wetu,  
Mwatubaka na kuapa, kutung'ata nyi' majitu.

Maisha hatujakopa, fahamu mkosa utu  
Hayo makeke na pupa, mtakoma utukutu,

8. Mtakoma utukutu, na kutumia mikiki,  
Na tabia zenyе kutu, tumechoka nay a chuki,  
Hatutakubali katu, kutendewa yenye haki  
Serikali fanya kitu, kwani nasi tuna haki

### **SHAIRI B**

Mwanadamu mambo yake, kueleweka muhali  
Ubavuni umuweke, umutowe kule mbali  
Maskanini afike, umtindie fahali  
Utamu anufaika, sima bada au wali  
Hatimaye ateuke, kwa viliwa nya samli  
Mwanadamu simuamini, afadhali nyama lumbwi

Mwanadamu umjenge, awe mwenhye kutajika  
Mambo yake uyapange, ukawa wahangaika  
Uwashe wake muwenge, uhakikishe wawaka  
Nao mkono umuunge, vyake view vyauungika  
Dhorubani umkinge, asipate kudhurika  
Mara atakusahau , wema wako kafukia

Mwanadamu mpe cheo, kuwa akutumikie  
Amani yako umpeo, fanaka uirajue  
Kwake iwe kimbilio, wamini akukwamue  
Mwisho takuwa kilio, shika sikio ujue  
Ndio wake mwelekeo, yauauma avuvie  
Mwanadamu mgeuze, pande zote umtizame

Mwanadamu mfadhili, kwa kila lililo jema  
Pasiwe hata dalili, ya kwake kukosa wema  
Viteko siwe akali, kumbizo zikaterema  
Binadamu takudhili, dhili zako kazitema  
Licha ya zote jamili, mwanadamju si muema  
Mwanadamu ni mtu, lakini nusu mnyama

## **Maswali**

- i. Linganisha mashairi haya:-
  - a) Kimuundo (Al. 3)
  - b) kibahari (Al. 3)
- ii. Tambua nafsineni katika shairi A. (Al. 2)
- iii. Andika ubeti wa pili wa shairi B kwa lugha tutumbi (Al. 4)
- iv. Fafanua tamathali nne za usemi zilizotumkiwa katika shairi la A. (Al. 4)
- v. Fafanua maudhui mawilimawili yanayojitokeza katika shairi A na shairi B. (Al.4)

7.

### **E. FASIHI SIMULIZI**

Aisei mmesikia hii kweli? Jamaa mmoja siku moja alilala fo fo fo baada ya kupiga mtindi hadi akachoka tiki! Alipofika kwake alipata mke amefura kama hamri. Kwa vile hakutaka mambo mengi, alienda moja kwa moja hadi kulala na akaanza kung'orota. Usiku wa manane uliposhika kani, msela huyu akaanza kuota kuwa yeye ni kuku na akaanza kutaga mayai kubwa kuuuubwa! Akataga yai la kwanza; akatua. Akataga la pili; akatua, alipokuwa anataga la tatu kwa nguvu zake zote, akapokea kofi moja kali na teke la ubavuni kutoka kwa mkewe. Akaamka huku akishangaa... mkewe akimlaani kwa matusi makali, “ Mbona unaninyea kama mtoto? Huwezi amka kwenda chooni? Mjinga wewe! Unalewa ovvovyo kisha kuja kujiendea haja kubwa matandikoni?”

- (a) Bainisha utanzu na kipera cha utungo huu kwa kutoa ithibati. (alama 2)
- (b) Jadili sifa nne za kipera ulichokitambua. (alama 4)
- (c) Umepewa nafasi ya kuigiza kipera hiki shulenii mwenu. Fafanua mambo manane ambayo utayaigiza kutoka kwenye kifungu hiki. (alama 5)
- (d) Eleza vikwazo vinavyozuia ukuaji wa fasihi simulizi (alama 5)
- (e) Jadili jinsi viziada lugha vitatumwiwa katika kukuza vipera mbalimbali vya fasihi simulizishulenii mwako. (alama 4)